

JE MNA CHAMA?



Majukumu na Faida

- Kuwapa sauti watoa huduma wa DLDM
- Kuwawezesha wanachama kiuchumi
- Kuimarisha ufuataji wa sheria kwa hiari ili kuboresha utoaji wa huduma
- Kuboresha uhusiano wa kikazi kati ya watoa huduma wa DLDM
- Kujenga na kuimarisha uhusiano na wadau wa DLDM
- Kuimarisha uendelevu wa mpango wa DLDM

**VYAMA VYA WATOA HUDUMA WA
DLDM NI NJIA BORA YA KUWAWEZESHA
WANACHAMA NA KUBORESHA
UTOAJI WA HUDUMA**

JE, MNAELEWA WAJIBU WA CHAMA?

FURAHAI YETU NI

DUKA LA DAWA MUHIMU



- Kuhamasisha ufuataji wa sheria na viwango kwa hiari
- Kuhamasisha matumizi sahihi ya dawa na kununua dawa kutoka kwenye vyanzo vinavyotambulika kisheria
- Kuwalinda wateja dhidi ya huduma zisizozingatia maadili kama vile kupanga bei ya pamoja isiyojali maslahi ya wateja
- Kulinda mpango wa DLDM dhidi ya wasimamizi wa sheria wanaokiuka wajibu wao kwa maslahi binafsi
- Kuhamasisha uwazi na uwajibikaji katika utoaji wa huduma

**VYAMA VYA WATOA HUDUMA WA DLDM
VINAWEZA KUCHANGIA KATIKA UTOAJI
WA HUDUMA BORA YA DAWA KWA JAMII**

JE, CHAMA CHENU KIMESAJILIWA?



Mahitaji

- Nakala mbili za katiba ya chama
- Muhtasari wa kikao kilichopitisha katiba ya chama
- Nakala mbili za fomu ya maombi (Form SA 1)
- Nakala mbili za taarifa kuhusu chama zilizojazwa kikamilifu kwenye fomu maalum (Form SA 2)
- Barua ya utambulisho kutoka kwa mamlaka husika
- Ada ya maombi Tsh.10,000
- Ada ya usajili Tsh.100,000
- Ada ya mwaka Tsh.40,000
- Nakala mbili za orodha ya wanachama waanzilishi wasiopungua kumi (10) pamoja na saini zao
- Barua ya maombi ipelekwe kwa Msajili wa Vyama vya Kijamii, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, S.L.P. 9223, Dar es Salaam

**USAJILI NDIYO NJIA PEKEE YA
KUTAMBULIKA KISHERIA**

JE, CHAMA CHENU KINA MIPANGO?




Hatua za Kupanga

- Ainisha dira yako
- Weka bayana dhamira ya chama
- Ainisha miongozo ya msingi ya chama
- Tathmini hali halisi ya chama
- Weka lengo kuu
- Ainisha malengo mahususi
- Weka mikakati ya utekelezaji
- Weka vipaumbele vya utekelezaji
- Tengeneza mpango kazi
- Weka mpango wa ufuatiliaji na tathmini

**KUWA NA MIPANGO NDIO NJIA
SAHIHI YA KUFIKIA MALENGO**

JE, CHAMA CHENU KINA MUUNDO WA UTAWALA?



Kupangilia

- Weka muundo wa chama
- Ainisha majukumu na wajibu wa watendaji
- Elezea njia za kuratibu shughuli za chama
- Elezea mfumo wa utoaji wa taarifa

**MUUNDO MZURI WA UTAWALA HUSAIDIA
MGAWANYO, URATIBU NA USIMAMIZI
BORA WA SHUGHULI ZA CHAMA**

JE, CHAMA CHENU KINA NGUVU KAZI?



Endapo chama kitaajiri watendaji:

- Amua idadi ya watendaji
- Ainisha sifa na ujuzi
- Mkubaliane juu ya taratibu za kuajiri
- Ainisha namna ya kutathmini waajiriwa
- Weka malipo yanayolingana na wajibu na uwezo wa chama
- Ainisha taratibu za kuachishwa kazi

**RASILIMALI WATU NI NGUZO KUU
KATIKA UENDESHAJI WA CHAMA**

JE, CHAMA CHENU KINA UONGOZI BORA?



Masharti ya Uongozi Bora

- Tayarisha sera zinazolingana na malengo ya chama
- Ainisha taratibu za utekelezaji wa sera
- Tayarisha mwongozo wa usimamizi wa shughuli za chama kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa
- Hakikisha watendaji wote wanaelewa taratibu na sera za chama
- Hakikisha shughuli zote za chama zinatekelezwa kwa kuzingatia taratibu na sera zilizowekwa

UONGOZI BORA HULETA UFANISI KATIKA USIMAMIZI WA CHAMA

JE, UONGOZI WA CHAMA UNAFUATILIA UFANISI WA WATENDAJI?




- Weka viwango vya ufanisi
- Pima na toa taarifa ya ufanisi
- Linganisha ufanisi halisi na viwango vilivyowekwa na ainisha upungufu
- Chukua hatua zinazofaa kuboresha ufanisi

**UFUATILIAJI WA UFANISI HUSAIDIA UTEKELEZAJI
WA SHUGHULI ZA CHAMA KULINGANA NA
TARATIBU NA SERA ZILIZOWEKWA**

JE CHAMA CHENU KINAENDESHWA VIZURI?



Shughuli za Usimamizi



**USIMAMIZI WENYE TIJA UNAHITAJI MIPANGO
MIZURI, MUUNDO WA UTAWALA, RASILIMALI WATU,
UONGOZI BORA NA UFUAMILIAJI WA UFANISI**